

# Taasisi ya Thirdmill

## Beji ya Kufuasa

*Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na jikane mwenyewe, ajitwike mslaba wake, kisha anifuata. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha.*

Luka 9:23-24

Ufuasi wa Kikristo ni kumfuata Yesu na kukua katika yeye na katika maisha yako ya Kikristo. Inaweza kuhusisha vitu vingi. Inaweza kuwa mabadiliko ya kitabia. Inaweza kuwa ni kukua katika ufahamu wetu kuhusu Maandiko Matakatifu. Inaweza kuwa ni kuendeleza maarifa muhimu katika kueneza upendo na ujumbe wa Kristo kwa watu wengine. Lakini jambo moja mtambuka ambalo linadumu siku zote ni kutembea na Yesu kwa kicho na unyenyekevu kama mwanafunzi na mfuasi wake. Na jambo hili tulifanya kwa pamoja. Ufuasi unaweza kuwa na sura tofauti kulingana na hitaji na mahali unapoishi. Katika beji hii, mtajadili kuhusu vingele muhimu vinavyohitajika katika kufuasa kulingana na mahali na jisni ya kufanya kwa wengine.

### Vipengele vya Beji – Mada za kujadili zitatokana na maeneo haya matatu:

**Utamaduni** – Ufuasi mahali unapoishi

**Kanisa** – Ufuasi mahali ambapo Mungu amekuita

**Binafsi** – Ufuasi mahali ambapo umefanyika kile ambacho Mungu amekuitia

### Mada za Kujadili:

1. Suala la Ufuasi linaonekanaje katika nchi yako?
2. Ni mambo gani ya msingi yanayohitajika katika kumfuasa mtu?
3. Watu wanbalika vipi kadiri wanavyokua katika mahusiano yao na Kristo?
4. Ni mifano gani iliyopo kwenye Maandiko ambayo tunaweza kutumia katika kuelezea namna ambavyo ufuasi unapaswa kuwa?
5. Ufuasi una sura gani sasa katika kanisa lako? Chora picha au kielelezo kinachoonesha hali ya ufuasi katika kanisa lako.
6. Andaa orodha ya mistari mitano ya Biblia ambayo inazungumzia ufuasi.
7. Ni maeneo gani katika maisha ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika kuandaa mpango wa ufuasi?
8. Ni amri ipi ambayo Yesu aliizungumzia katika Yohana 15?

9. Ni kwa jinsi gani ufuasi unahusika na madiliko ya tabia au kukuza tunda la Roho Mtakatifu?
10. Unapaswa kufuasa watu wangapi kwa mara moja?
11. Biblia ina nafasi gani katika mchakato wa kufuasa (kusoma, kujifunza, kukariri n.k.)?
12. Mambo yana nafasi gani katika kufuasa?
13. Kuna uhusiano gani kati ya kufuasa na kuandaa viongozi katika kanisa lako?
14. Nini kinamfanya mtu mmoja kufuzu na kumfuasa mwingine? Unajuaje kuwa umeweza kumfuasa mtu inavyotakiwa?
15. Ni jinsi nyinyi wote ‘mnanena’ na ‘kuonyesha’ katika hatua za kufuasa.
16. Ni kwa jinsi gani unatawawezesha wafuasi wako ili nao wawafuase wengine na siyo kuwa wafuasi tu?
17. Ni kitu gani kinakupa hamasa katika kupenda na kujitoa kwa Yesu, na unawezaje kuhusianisha hilo na kuwafuasa wengine?
18. Ni kitu gani kinaimarisha au kupunguza nguvu ya dhambi katika maisha yako?
19. Ni matendo gani au nidhani ipi imekuwa msaada kwako katika jitihada za kumuishia Kristo?

### **Mambo ya Kufanya:**

1. Toa taarifa juu ya mambo yote ambayo Bwana ametenda katika maisha yako na kukutengeneza kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Pia toa taarifa juu ya mambo ambayo unatamani ayafanye kwako kwa miaka kumi ijayo.
2. Toa taarifa ya mambo yote ambayo kanisa lako linafanya katika kufuasa watu wake. Mwisho mwa mjadala katika kikundi chako, wasilisha mpango wa kanisa lako au huduma yako wa kufuasa kulingana na mazungumzo yenu.
3. Anza mara moja kumfuasa muumini mwingine.

### **Vigezo vya Beji:**

Utatunukiwa Beji hii na tasisi ya Thirdmill kama sehemu ya Cheti cha Misingi baada ya kufuzu vigezo vyote vya Beji vilivyo kwenye *mambo ya kufanya* kwa uaminifu, na *uthabiti*, kwa kufuata *vipengele vya Beji*, na muktadha wa *mada zilizozungumziwa* katika kipindi chote cha kozi.